MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

JARIDA LA HALI YA HEWA

Na. 41 Toleo maalumu: Utabiri wa mvua za Novemba, 2026 hadi April, 2027 (NDJFMA) Imetolewa: Tarehe 23 Oktoba, 2026

- Mvua za Msimu 2026/2027 zinatarajiwa kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na hali ya El Niño inayotarajiwa, hususan nusu ya kwanza ya msimu (Novemba 2026 hadi Januari 2027).
- Mvua za juu ya wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Hata hivyo, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi.
- Mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2026 katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Lindi na Mtwara na kusambaa katika maeneo mengine mwezi Novemba 2026. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027 katika maeneo mengi.
- Mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2026-Januari, 2027), ikilinganishwa na nusu ya pili (Februari -Aprili, 2027).

MIFUMO YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MSIMU WA MVUA CHA NOVEMBA, 2026 HADI APRIL, 2027

Katika kipindi hiki cha msimu wa mvua, joto la bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la juu ya wastani, hali inayoashiria mwendelezo wa uwepo wa *El Niño* yenye nguvu kubwa. Aidha, joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi ikilinganishwa na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba 2026 hadi Januari 2027), hali inatarajiwa kusababisha upepo wa bahari wenye unyevu kuvuma kuelekea maeneo ya nchi yetu. Vilevile, joto la bahari la Juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

Vilevile, upepo wa magharibi wenye unyevunyevu unatarajiwa kuvuma kutoka misitu ya Kongo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi na ukanda wa kati na hivyo kuimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU NOVEMBA, 2026 HADI APRIL 2027

Mvua za Msimu ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa, mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Hata hivyo, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi na zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Lindi na Mtwara na kusambaa katika maeneo mengine mwezi Novemba 2026. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027 katika maeneo mengi.

Mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2026-Januari, 2027), ikilinganishwa na nusu ya pili (Februari-Aprili, 2027). Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

Kanda ya magharibi (mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma):


Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2027.

Kanda ya Kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):
Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):
Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2027.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Lindi na Mtwara):
Mvua wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027.

Maeneo ya kusini mwa nchi (Mkoa wa Ruvuma):
Mvua wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Desemba, 2026. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027



Kielelezo: Mwelekeo wa mvua za Msimu (November, 2026 had April, 2027)

ATHARI NA USHAURI

Kilimo, mifugo, uvuvi na wanyamapori

Mvua za wastani hadi juu ya wastani na juu ya wastani hadi wastani katika meneo haya zinazotarajiwa kuchangia ongezeko la vipindi vya unyevunyevu mwingi kupita kiasi kwenye udongo, kutuama kwa maji na mafuriko na kuathiri ukuaji wa mazao na uharibifu wa miundombinu ya kilimo. Aidha, magonjwa ya mazao yanayosababishwa na fangasi, bakteria na virusi yanatarajiwa kuongezeka. Magonjwa hayo yanaweza kuathiri ukuaji, ubora na mavuno ya mazao mbalimbali, hususan viazi mviringo, alizeti, maharage, ufuta, matunda na mbogamboga. Shughuli za uvunaji, ukaushaji, usafirishaji na uhifadhi wa mazao zinatarajiwa kuathirika kutokana na mvua za muda mrefu na hivyo kuongeza hatari ya upotevu wa mazao baada ya kuvuna. Aidha, wakulima wanashauriwa kutumia mbinu na teknolojia bora za kilimo ikiwemo kuanda mifereji, kilimo cha kontua na matuta ili kuzuia kutuama kwa maji mashambani, mmomonyoko wa udongo na upotevu wa rutuba ya udongo.

Wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kunufaika na ongezeko la upatikanaji wa malisho ya mifugo na chakula cha samaki, hivyo kuongeza uzalishaji. Hata hivyo, unyevunyevu mwingi na maji yaliyotuama vinaweza kuongeza hatari ya milipuko ya magonjwa ya mifugo, kama vile homa ya bonde la ufa na kuoza kwa kwato, pamoja na kuongezeka kwa wadudu wanaosambaza magonjwa. Aidha, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia ushauri kutoka kwa maafisa ugani, na kuchukua hatua stahiki, ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuongeza tija katika msimu huu wa mvua.

Upatikanaji wa malisho na maji kwa wanyamapori katika mbuga na hifadhi unatarajiwa kuwa mzuri. Hata hivyo, mvua nyingi zinazotarajiwa zinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko, ambayo yanaweza kusababisha wanyamapori kuhama, maambukizi ya magonjwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa wanyama wanaofugwa kutokana na wanyamapori kuingia katika maeneo ya jamii yanayozunguka hifadhi na mapori ya akiba. Hali hiyo inaweza kuongeza kwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori, na kusababisha hatari kwa binadamu na wanyama wanaofugwa. Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu kama vile barabara na mikondo ya kupitisha maji katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa.

Angalizo 2: *Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha mvua za Msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na utabiri wa kila mwezi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).*

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)